**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/NZ/2024/39**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2025-00000016**

**KATI YA**

**KEPHAS DAUDI MOLLEL ..........................................................MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ........................ MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 145 cha tarehe 12 mwezi Februari 2025)***

## 1.0 <u>Maelezo ya Awali</u>

Mnamo tarehe 17 Disemba 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Kephas Daudi Mollel wa Wilaya ya Arumeru - Jijini Arusha, ("Mlalamikaji") dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji anamtaka Mlalamikiwa kuhamisha miundombinu yake (nyaya) zilizopitishwa juu ya eneo la Mlalamikaji lililoko Kitongoji cha Ikrevi, Kata ya Oltroto, Tarafa ya Enaboishu Wilaya ya Arumeru jijini Arusha bila ridhaa yake.

Mlalamikaji anaeleza kwamba, eneo hilo analimiliki kwa zaidi ya miaka arobaini (40). Mnamo tarehe 13 Novemba 2024, mafundi wa Mlalamikiwa walifika katika eneo hili na kubadilisha nguzo na nyaya bila ridhaa ya Mlalamikaji, na kwamba, hata alipojaribu kuzuia zoezi hilo lisiendelee hakufanikiwa.

Mlalamikaji anaeleza zaidi kwamba, hata hapo awali hakuwahi kuridhia upitishwaji wa miundombinu ya Mlalamikiwa (nyaya) katika eneo lake. Mlalamikaji aliwasilisha malalamiko yake ofisini kwa Mlalamikiwa lakini hakupata majibu, ndipo alipoamua kuwasilisha Malalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA) na kuiomba Mamlaka kumuamuru Mlalamikiwa kuhamisha miundombinu (nyaya) kwa gharama zake.

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 20 mwezi Disemba 2024, Mamlaka (EWURA), ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro TS Na. 428/2020 - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake tarehe 7 Januari 2024, na kuieleza Mamlaka kwamba, walifanya tathmini ya kiini cha mgogoro na kufikia muafaka kwamba watahamisha nyaya ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya majibu ya utetezi.

Kikao cha usuluhishi kati ya wadaawa kilichofanyika tarehe 21 Januari 2025, katika ukumbi wa mikutano wa ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini jijini Arusha. Mwisho wa kikao cha usuluhishi, pande zote mbili zilikubaliana kwamba:

a) Mlalamikiwa atahamisha miundombinu yake (nyaya) kwa gharama zake katika eneo la Mlalamikaji ifikapo tarehe 21 Februari 2025,
b) Mlalamikaji atatoa eneo lake kidogo ili Mlalamikiwa aweze kuhamishia nguzo pamoja na waya shikizi (*stay way*).

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba;

a) Mlalamikiwa atahamisha miundombinu yake (nyaya) kwa gharama zake katika eneo la Mlalamikiwa ifikapo tarehe 21 mwezi Februari 2025.

b) Mlalamikaji atatoa eneo lake kidogo ili Mlalamikiwa aweze kuhamishia nguzo pamoja na waya shikizi (*stay wire*).

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 12 mwezi Februari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**